# ICAN

## Tathmini ya Kimataifa ya Kuhesabu

Tathmini ya chanzo huru iliyoandaliwa kupitia ushirikiano wa nchi za kusini kuendana na malengo ya Maendeleo Endelevu SDG 4.1.1a



## Hali halisi ya sasa na kuongezeka kwa shida ya kujifunza

Janga la ugonjwa wa Korona-19 (COVID-19) limeathiri jamii kote ulimwenguni. Ili kusaidia kudhibiti kuenea kwa virusi, shule ulimwenguni kote zilifungwa na kuathiri zaidi ya wanafunzi bilioni 1.5.

Kabla ya mshtuko uliosababishwa na janga hili, karibu watoto milioni 260, na vijana tayari walikuwa nje ya shule. Hata miongoni mwa wale walioandikishwa, wengi wao hawakupata hata ujuzi wa msingi wa kusoma na kufanya hesabu rahisi.

Kufungwa kwa shule na usumbufu mwingine kwasababu ya janga la Korona kutasababisha kudhoofisha zaidi ujifunzaji, kuongezeka kwa wanafunzi wanaoacha masomo na kukosekana kwa usawa zaidi. Wakati watoto hawaendi shule, karibu tafiti na tathmini zote za ujifunzaji zimesitishwa pia, na kuzidisha changamoto ya kupata takwimu za kuaminika juu ya ujifunzaji, hasa makundi yenye mazingira magumu na yaliyotengwa. "

## Inaweka Msisitizo kwenye ahadi ya SDG

Matokeo ya kujifunza yameelezwa kwa wazi katika Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDG) lengo la 4. shabaha na 4.1 linasema: " Kufikia mwaka 2030, hakikisha kwamba wasichana na wavulana wote wanamaliza elimu ya msingi na ya sekondari ya bure, yenye usawa na bora itakayowapatia matokeo bora ya kujifunza. " Pamoja na msisitizo wa SDG, kufungwa kwa shule kwasababu ya COVID-19 kunaweza kubadilisha mafanikio yoyote yaliyopatikana hadi sasa, hasa kwa watoto wadogo. Kama ujuzi wa msingi haujengwi katika hatua za mwanzo za kujifunza, uwezekano wa kuendelea vizuri madarasa ya juu ya elimu ya msingi ni mdogo.

Ili kubaini mapungufu yaliyopo kwa watoto madarasa ya awali , SDG 4.1.1 (a) inapima wastani wa idadi ya watoto wa darasa la 2 au la 3 wanaojua na kumudu angalau kiwango cha chini cha ujuzi wa kusoma na kuhesabu. Ufuatiliaji wa maendeleo chini ya kiashiria hiki unahitaji tathmini madhubuti, ya mara kwa mara, na inayolinganisha matokeo ya msingi ya ujifunzaji wa watoto (ndani ya nchi kwa muda fulani na vile vile kimataifa).

## Tathmini ya Kimataifa ya Kuhesabu

ICAN ni chanzo huru cha zana za tathmini iliyo makini na rahisi kutumia, inapatikana katika lugha 11, ambayo inatoa ulinganifu wa kimataifa wa matokeo ya kujifunza na inaendana na Malengo ya Maendeleo endelevu SDG 4.1.1 (a). ICAN iliandaliwa kupitia juhudi za pamoja kwa mashirika wanachama wa Mtandao wa PAL katika nchi 13 za kipato cha chini na cha kati zilizoko Afrika, Asia na Amerika.

## Kuna hitaji la haraka la tathmini inayolenga kupima ujuzi wa msingi wa wanafunzi wa awali

Mifumo yote ya elimu inatarajia watoto wapate uwezo wa msingi wa kusoma na kuhesabu katika miaka michache ya kwanza ili waweze kuwa na uwezo wa kujifunza maudhui magumu zaidi wanapoendelea na madarasa ya juu. Kwa sehemu kubwa, ufundishaji wa darasani unaongozwa na hitaji la kumaliza mtaala ulioandaliwa. Ingawa idadi kubwa ya watoto huwa nyuma ya matarajio ya mtaala, mara chache hupewa fursa ya kujifunza hadi waweze kumudu stadi hizi muhimu.

COVID-19 inaweza kusababisha msingi wa ujifunzaji kushuka zaidi kwa watoto wa madarasa ya mwanzo kwasababu ya kukosa msaada wa kimasomo nyumbani, hasa katika kaya zenye kipato duni.

## Vipengele & Kazi za ICAN

**50%**

**MAARIFA YA NAMBA**

- kuhesabu, kulinganisha idadi ya vitu
- Kutambua namba
- Kutoa na kujumlisha (kwa makundi na bila makundi)
- jaribio la maisha ya kawaida

**50%**

**JOMETRI**

- Nafasi & mwelekeo
- Maumbo & michoro

**VIPIMO**

- Urefu & uwezo/ umahiri
- Muda & Kalenda

**KUONESHA TAKWIMU**

- Kukumbuka taarifa rahisi

## ICAN inapima nini?

Kuna makubaliano mapana kwamba Msingi wa Kuhesabu unajumuisha vipengele kama vile kutambua namba, jiometri, vipimo na kuonesha takwimu rahisi.

Kiwango cha chini cha ujuzi wa kuhesabu kwa mujibu wa malengo ya maendeleo endelevu SDG 4.1.1 kwa darasa 2/3 pia unawataka wanafunzi kuonesha ujuzi wa kujua idadi, kutoa na kumlisha, kutambua maumbo na mielekeo.

Majaribio ya tathmini ya ICAN yameandaliwa kuendana na Mwongozo wa ujuzi wa Kimataifa wa UNESCO unaelekeza viwango vya chini vya ujuzi ambavyo wanafunzi wanatarajiwa kuwa navyo na kuvionesha.

## ICAN inatekelezwaje na Wapi?

ICAN inafaa kutumika kwenye mazingira ya shule au nyumbani. Uthibitisho mkubwa wa wazo hili umetekelezwa. Taratibu za ukusanyaji wa takwimu zilifuata Viwango vya Ubora wa Takwimu vya mwongozo wa mtandao wa PAL ambao unahakikisha unaendana na taratibu nzuri za tathmini za kidunia.

Ilifanyika katika nchi 13. Jamii 60 zilichaguliwa kinasibu kwenye wilaya 1 ya kijijini kwa kila nchi

Tathmini ilifanywa kwenye kaya zilizochaguliwa kinasibu kwa watoto wenye umri kati ya miaka 5-16

Kila mtoto alipimwa mmoja mmoja kwa kuulizwa maswali ana kwa ana kwa mdomo, ili kuepuka kudhani kwamba wanaweza kusoma au kuandika

Pia taarifa kuhusu watoto kusoma shule au la, elimu ya wazazi wao, kaya na miundombinu ya jamii zilikusanywa ili kuelewa kwa mapana masuala ya usawa na haki katika elimu

## Nchi iliko ICAN na mashirika yanayotekeleza





### Maeneo inakofanyakazi ICAN

| Mabara | Nchi | Wilaya za vijijini | Vijiji | Kaya 15,000+ | Watoto 15,000+ |
|---|---|---|---|---|---|
| 3 | 13 | 13 | 779 | na zaidi | na zaidi |

## Ukweli Muhimu kuhusu zana za tathmini za ICAN

- Ni chanzo huru; sasa inapatikana katika lugha 11
- Kazi nyingi za majaribio ya watoto zimepangwa kwa kiwango cha daraja la 3 au ya chini, kuendana na Mwongozo wa UNESCO wa Ujuzi
- Inawezekana kutumika kwenye tathmini zinazofanyika kwenye kaya na shuleni
- Inafaa kwa wanafunzi wa rika mbalimbali, ili kutambua mapungufu yao kwenye Hisabati
- Inafanywa kwa kuongea na mtu mmoja mmoja ikiwajumuisha watoto wote, hata wale ambao bado hawawezi kusoma kwa ufasaha
- Wastani wa muda wa tathmini ni dakika 15 kwa kila mtoto
- Inaendeshwa kwa kuzingatia uwezo wa mtoto - watoto wanaoweza kufanya kazi rahisi za kuhesabu ndio hupewa kazi za kiwango cha juu zaidi
- Inawezekana kutekelezwa sehemu kubwa ya nchi mazingira yenye rasilimali chache




PAL NETWORK People's Action for Learning


## ZANA ZA ICAN

## SETI YA 1


**Q1** Kwenye picha hii, paka yupi yupo ndani ya boksi?




**Q2** Kwenye picha hii, mtoto yupi yupo mbali zaidi na mti?



**Q3** Kwenye picha hii, kalamu ipi ni fupi zaidi?




**Q4** Hapa kuna mipira yenye ukubwa sawa. Angalia ukubwa wa maboksi kwa umakini. Kama kila boksi litajazwa ni mipira hiyo, boksi lipi litakuwa na idadi kubwa ya mipira?



# SETI YA 1

Angalia jedwali hili kwa umakini.





**Q5** Kuna mapeazi mangapi?


**Q6** Ndizi zimezidi idadi ya machungwa kwa ngapi?

Ni muda gani unaoneshwa kwenye saa hizi?

**Q7**



**Q8**



Angalia kalenda hii.

**MACHI 2019**


| JUMAPILI | JUMATATU | JUMANNE | JUMATANO | ALHAMISI | IJUMAA | JUMAMOSI |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | 1 | 2 |
| 3 | 4 | 5 | 6 | 7 | 8 | 9 |
| 10 | 11 | 12 | 13 | 14 | 15 | 16 |
| 17 | 18 | 19 | 20 | 21 | 22 | 23 |
| 24 | 25 | 26 | 27 | 28 | 29 | 30 |
| 31 | | | | | | |

**Q9** Tarehe 5 Machi ni siku gani ya wiki?


**Q10** Jumatatu ya pili ya mwezi ni tarehe ngapi?

## SETI YA 1


**Q11** Upi ni mstari mnyoofu kati ya mistari ifuatayo?



**Q12** Angalia haya maumbo, umbo lipi ni pembetatu?




**Q13** Kuna jumla ya ndege wangapi? Chagua jibu sahihi



6 8 9 5

**Q14** Angalia kwa makini makundi haya manne ya vitu. Je kundi lipi lina vitu vingi zaidi?



PAL NETWORK
People's Action for Learning

## SETI YA 2

**Q15** Tambua namba.

| | | |
|---|---|---|
| 3 | | 2 |
| | 8 | |
| 0 | | 9 |

Angalau namba 4 kati ya 5 ziwe sahihi

Fanya maswali yafuatayo.

**Q16**

$$\begin{array}{r} 32 \\ +\ 15 \\ \hline \\ \hline \end{array}$$

**Q17**

$$\begin{array}{r} 46 \\ -\ 21 \\ \hline \\ \hline \end{array}$$

**Q18**

$2 \times 4 =$

**Q19**

$9 \div 3 =$

## SETI YA 3

**Q20** Tambua namba.

| | | |
|---|---|---|
| 48 | | 22 |
| | 84 | |
| 97 | | 30 |

Angalau namba 4 kati ya 5 ziwe sahihi

Fanya maswali yafuatayo.

**Q21**

$$\begin{array}{r} 56 \\ +\ 17 \\ \hline \\ \hline \end{array}$$

**Q22**

$$\begin{array}{r} 78 \\ -\ 29 \\ \hline \\ \hline \end{array}$$

**Q23**

$$\begin{array}{r} 42 \\ \times\ 6 \\ \hline \\ \hline \end{array}$$

**Q24**

$7\overline{)93}$

**Q25** Sikiliza swali kwa makini, kisha fanya na utoe jibu.

Kuna watoto 43 uwanjani. Kati ya hao, watoto 25 wameenda nyumbani. Je watakuwa wamebaki watoto wangapi uwanjani?

**Q26** Sikiliza swali kwa makini, kisha fanya na utoe jibu.

Muuza duka ana maembe 48. Anahifadhi maembe 3 katika kila kasha. Je atahitaji makasha mangapi kama hayo ya kutosha maembe yote?



## Kuhusu PAL Network

Mtandao wa People's Action for Learning (PAL ) Network ni mtandao wa ushirikiano wa mashirika ya ukanda wa kusini mwa dunia yanayofanya kazi katika mabara matatu. Mashirika ya wanachama hufanya tathmini zinazoongozwa na wananchi wenyewe / au kuchukua hatua zinazoongozwa na wananchi wenyewe zinazolenga kuboresha matokeo ya kujifunza. Kuanzia mwaka 2005 na kuendelea, wanachama wa mtandao huu wamejikita kupima kama watoto walio na umri wa kusoma shule ya msingi wanaweza kusoma maandishi rahisi na kufanya hesabu rahisi. Pia katika maeneo mengi washirika wa mtandao wa PAL hutekeleza programu na mipango kazi inayolenga kuhakikisha kuwa watoto wote wanapata stadi hizi za msingi.

CLAs/tathmini inayoongozwa na wananchi ni tathmini inayofanyika katika kaya na ya ana kwa ana kwa kuzungumza na kila mtoto. Tathmini hizi kwa kawaida hufanywa na sampuli ya uwakilishi wa watoto katika mkoa / jimbo au kitaifa na kurudiwa mara kwa mara baada ya muda fulani. Jitihada hizi zinaongozwa na taasisi za kitaaluma au asasi za kiraia na zinajumuisha ushiriki wa wadau wengi mbali mbali katika kila nchi.



**Kwa taarifa zaidi, tembelea:**

www.palnetwork.org

info@palnetwork.org

PAL Network

palnetworkHQ

PAL NETWORK
People's Action for Learning